**Sikiliza na Ujifunze - Mazingira na Hali ya Hewa**
**08 – Desertification (Kuenea kwa jangwa)**
**Text: Richard Lough**
**Redaktion und Idee: Johannes Beck**
**Translator: Mohamed Dahman**

---

Hujambo msikilizaji! Karibu katika mfululizo wa vipindi maalum vya Sikiliza na Ujifunze kuhusu mazingira. Leo hii tutakuwa na habari za kuenea kwa haraka kwa jangwa barani Afrika kutokana na harakati zetu wenyewe binaadamu kuweka shinikizo kubwa kwa ardhi. Uchungaji wa wanyama kupindukia na ukataji wa misitu unaigeuza ardhi kavu na ile ilio nusu kavu ya Afrika kuwa ardhi isioweza kuzalisha kitu kwa kupitia mchakato unaojulikana kama ardhi kugeuka jangwa. Leo radionovela itaangalia vipi wakulima wadogo halikadhalika wakubwa wanavyoruhusu uchungaji wa mifugo yao kuifanya ardhi kuwa tupu kabisa. Jambo hili husababisha uharibifu kwa udongo ambao utadumu kwa miongo kadhaa na kuchangia moja kwa moja kuenea haraka kwa jangwa barani Afrika.

**Music – 0:30**

**SFX local restaurant ………mkahawa wa kienyeji**

| | |
|---|---|
| **Monica:** | Unajua sisi Waafrika tunaweza kuwa watu wa kuchekesha sana wa maajabu. Angalia wazunngu wao wanawekeza utajiri wao kwenye mali wakati sisi tunawekeza utajiri wetu kwenye wanyama …. ng’ombe, mbuzi, ngamia na kadhalika. |
| **Moses:** | Lakini wakati nitakapofunga ndoa vipi nitaweza kuipa familia ya mke wangu nyumba! Hapana lazima iwe mifugo… hasa ng’ombe iwapo nitamudu au vinginevyo itakuwa mbuzi… |
| **Monica:** | (Laughs … anacheka ) Moses una mambo ya kizamani sana. Bado unafikiri kwamba unaweza |

kulipa mahari ya biharusi… katu hutomudu kulipa ng'ombe wa kutosha kwa ajili yangu!

**Moses:** Nadhani baba yako atakubali ng'ombe 20. Yeye ni mtu wa mila.

**Gladys:** (Hum of agreement - mguno wa kukubali) Hmmm ni kweli baba yangu pia ni hivyo hivyo. Hivi karibuni baba yangu amenunua mifugo ya mbuzi ili kwamba aweze kuwapa wakwe wa kaka yangu mahari yao …umeipata hapo … mbuzi hamsini wakiwemo mabeberu 10!

**Moses:** Lakini baba yako tayari ana zaidi ya mbuzi mia moja kwenye shamba lake na ana ng'ombe pia! Vipi anaweza kupata malisho mazuri kwa wanyama wengi kiasi hicho?

**Gladys:** Sio rahisi. Kiwango cha ubora wa nyasi kinazidi kuwa kibaya…

**X –fade restaurant into SFX birdsong and intermittent SFX Goats ……ondowa sauti ya mkahawani na kuingiza sauti ya ndege na mbuzi**

**Monica:** Hee! Gladys shamba lenu linaonekana tofauti sana!

**Gladys:** (sounding puzzled ……akionekana kubabaika ) Una maanisha nini? Hakuna kitu kilichobadilika hapa. Ohhh … isipokuwa misitu imekwenda…

**Moses:** Monica yuko sahihi. **(SFX walking on bare soil …wakitembea kwenye udongo mkavu)** Ardhi hapa ilikuwa imejaa vichaka na miti midogo na nyasi zilikuwa rangi kijani kibichi.

**Gladys:** Baba yangu aliisafisha ardhi miaka mitano iliopita. Alikuwa akihitaji ardhi zaidi kwa uchungaji kwa hiyo aliiunguza yote.

**Monica:** Huwa wanauita utaratibu huo wa kufyeka na kuunguza. Nimejifunza juu ya utaratibu huo katika darasa la geografia wiki iliopita. Wafugaji wanaohitaji ardhi zaidi ya uchungaji hukata maeneo ya misitu na kuyaacha yakauke. Baada ya muda fulani wakati mimea inapokuwa imekauka mkulima huiunguza kwa ajili ya kuwa na konde aidha kwa ajii ya mazao au ufugaji.

**SFX approaching footsteps … hatua za miguu zikikaribia**

**Moses:** Habari za mchana Bw. Wambula …

**Bw.Wambula:** (Grunt of acknowledgment ……mguno wa kukiri) Hmmm … Vipi unashangaa na mifugo mipya?

**Moses:** Ndiyo bwana. Gladys alikuwa akituambia kwamba umeongeza ukubwa wa shamba lako miaka michahe iliopita.

**Bw. Wambula:** Ahhh …ndiyo wakati familia inapoongezeka unahitaji mifugo zaidi kujikimu.

**SFX hum of agreement ….mguno wa kukubali**

**Bw. Wambula:** Mimi na majirani zangu tuliitia moto miti na kusafisha kama hekta ishirini za ardhi. Tulifikiri kwamba nyasi zitaota tena kwa nguvu na kwa wingi zaidi… (sigh of resignation …mguno wa kukata tamaa)… lakini mnaweza kujionea wenyewe hali sio nzuri hivi sasa…

**Moses:** Ni vumbi tupu nyasi haziko kabisa katika hali ya kawaida zimekuwa kama viraka vya hapa na pale …

**Josephat:** (approaching voice … sauti inayowasogelea) Habari gani baba…

**Bw. Wambula:** Ahaa … huyu ni mwananagu Josephat ni kaka wa Gladys.

**Moses/ Monica:** Habari gani?

**Bw.Wambula:** Josephat yuko katika chuo cha Kilimo, fursa ambayo mimi mwenyewe sikuwahi kuipata…

**Monica:** Je Josephat unaweza kutuelezea kwa nini ardhi ya baba yako ni mbaya sana?

**Josephat:** Unajua kwanza kabisa wakati unapokata miti sehemu ya juu ya udongo inakuwa rahisi kuathirika na upepo na mvua. Bila ya kuwepo kwa mizizi ya miti na vichaka kushikilia udongo pamoja inakuwa rahisi kwa udongo huo kusombwa na maji wakati wa mvua kubwa. Halikadhalika virutubishi vyote vilivyomo kwenye sehemu hiyo ya juu ya udongo.

**(collective Ahhh of understanding … sauti ya pamoja ya Ahaaa kuonyesha kufahamu)**

**Bw. Wambula:** Lakini Josephat niliipa muda ardhi kurudi kwenye hali yake ya kawaida… niliacha nyasi ziote tena.

**Josephat:** Ndiyo baba ulifanya hivyo lakini udongo ulikuwa umedunishwa. Hii ina maana kusema kwamba umekuwa hauna rutuba kama ilivyokuwa hapo awali. Halafu wakati ulipoanza kuchunga mifugo kulikuwa na kile tunachokiita shinikizo zaidi juu ya udongo huo.

**Moses:** (confused …akionekana kuchanganyikiwa) Vipi unaweza kuishinikiza ardhi?

**Josephat:** Ndiyo… hebu niambie wale mbuzi pale pembeni wanafanya nini?

**SFX Hooves scrapping ground …kwato za mbuzi zikikwangua udongo**

**Moses:** Wanakwanura tu udongo kwa kutumia kwato zao.

**Josephat:** Umesema wanakwangua tu… lakini nini athari yake?

**Monica:** Wanatimua vumbi.

**Josephat:** Lakini vumbi ni kitu gani?

**Monica/ Moses:**(together …kwa pamoja ) Hatujuwi.

**Josephat:** Vumbi ni chembe nduchu sana za udongo…Kila wakati pale mbuzi anapopiga kwato zake kwenye ardhi hugandamiza udongo na kuufanya uwe mgumu. Juu ya udongo huo kuna safu ya vitu laini… kile ambacho unakiona mbuzi wakikipiga mateke hiyo ni aina nyengine ya mmommonyoko wa ardhi. Ziada ya hilo wakati mvua inaponyesha maji hayawezi kupenya juu ya udongo ulioathirika uliogandamizwa. Kwa hiyo badala yake maji hayo hutembea juu ya ardhi na kusomba udongo uliokuwa haukushikamana.

**Bw.Wambula:** Unasema wakati mvua inaponyesha… lakini Josephat kwa miaka miwili kumekuwa hakuna mvua (Exclaims… anatamka kwa hasira) Tuko katika ukame!

**SFX manual water pump ……bomba la kuvuta maji kwa mkono**

**Bw.Wambula:** Hivi ndivyo ninavyowapatia maji wanyama wangu kwa kuvuta maji kutoka kwenye kisima. Ni ukame unaopaswa kulaumiwa na sio wanyama wangu.

**Gladys:** Kwa hakika anayosema ni kweli! Vipi nyasi zinaweza kuota wakati mvua ikiwa ni haba?

**Josephat:** Kwa kweli baba hauko sahihi moja kwa moja.

**Bw. Wambula:** Alaaa… tuambie kwa nini?

**Josephat:** Ni kueleweka vibaya ambako kumekuwa kwa kawaida kwamba ukame wenyewe ndio unaosababisha kuenea kwa jangwa. Ni kweli ukame ni sababu. Lakini sababu kuu ni binaadamu kuyatumia vibaya mazingira. Ndiyo, tumekumbwa na ukame fulani kwa miaka miwili iliopita… sikatai… lakini sio kusema kwamba kulikuwa hakuna mvua kabisa. Na ardhi hapa ikiwa itasimamiwa vyema inaweza kurudi kwenye hali yake ya kawaida.

**Bw. Wambula:** (indignatly …tamka kwa hasira ) Mimi nimeisimamia ardhi vizuri!

**Josephat:** Hebu nikuulize suala hili. Kabla ya kuchimba kisima wapi ulikuwa ukichunga wanyama?

**Gladys:** Nakumbuka ulikuwa ukizunguka. Ulikuwa mfugaji wa kutangatanga. Ulikuwa ukizifuata mvua na malisho mazuri.

**Bw. Wambula:** Ndiyo, nilikuwa nikifanya hivyo.

**Moses:** Ahaaa…kumbe ulikuwa ukichunga mifugo kwenye eneo moja na baadaye kwenda jengine na jambo hilo huupa udongo na mimea muda wa kurudi katika hali yake ya kawaida.

**Josephat:** Hasa!

**Bw. Wambula:** Lakini sasa sina haja ya kuzunguka kwa sababu kisima kinakuwa na maji daima.

**Josephat:** Sawa… kwa hiyo ardhi hapa inakuwa kwenye malisho mfululizo na inakuwa haina nafasi ya kurudi kwenye hali yake ya kawaida. Sio kosa lako baba. Ukweli wa mambo ni kwamba wakati idadi ya watu wetu ikiongezeka kunakuwa na nafasi haba kwa kila mtu na mahitaji yanakuwa makubwa kwa ardhi.

**Monica:** Lakini je shamba la baba yako linaweza kuwa na mimea tena na lenye rutuba?

**Josephat:** Inawezekana kwa kupitia mchakato wa asili juu ya kwamba itachukua muda mrefu… miongo kadhaa pengine sio hata katika maisha yetu sisi. Lakini ili hilo lifanyike inabidi aache kuchunga wanyama wake hapa.

**Gladys:** Unaonekana mwenye matumaini.

**SFX walking over bare ground ……wakitembea juu ya ardhi kavu**

**Josephat:** Tatizo ni kwamba baba yetu sio peke yake. Mahala hapa pote tunashuhudia kuendelea kudunishwa kwa ardhi. Jambo hili hili linatokea nchi nzima halikadhalika bara zima.

**(collective 'oh' of suprise ……. tamko la pamoja la mshangao Oohh )**

**Josephat:** Wakati ardhi inapokuwa tupu kunakuwa hakuna miti na mimea ya kushikilia unyevu ulioko hewani kwa hiyo mvua huwa haba. Kile tunachokisikia ni kwamba utakuja wakati ambapo kutakuwepo kwa mabadiliko ya kudumu ya nyendo za hali ya hewa.

**Monica:** Una maana kwamba iko siku ardhi hii inaweza kuwa jangwa?

**Josephat:** Ndiyo, pale hali itakapokuwa mbaya kabisa… lakini hayo tayari yanatokea barani kote Afrika.

**Music: 0:30**

**Je ulikuwa ukijua?**

Je ulikuwa ukijua kwamba katika ngazi ya dunia watu bilioni moja nukta mbili wako hatarini kutokana na ardhi kugeuka jangwa. Idadi hiyo ni sawa na mtu mmoja katika kila kundi la watu sita. Inaaminika kwamba asilimia 75 ya ardhi kavu kabisa duniani yaani kama kilomita za mraba milioni 45 zinaathirika kwa kugeuka jangwa.Kila mwaka kama hekta milioni sita za ardhi ya kilimo hupotea na kugeuka jangwa moja kwa moja. Ardhi kugeuka jangwa sio jambo jipya. Kwa kweli staarabu kadhaa za kale ikiwa ni pamoja na himaya ya Babylonia zimedhoofika kwa haraka sana baada ya mazao yao ya kilimo kupunguwa kutokana na uhaba wa maji.

Lakini kuenea kwa jangwa kwa hivi sasa kunafanyika kwa haraka sana kuliko ilivyotokea kihistoria.Suala nani anahusika na hili? Naam lawama moja kwa moja zinatuangukia sisi wenyewe. Harakati za binaadamu kama vile ukataji wa miti na uchungaji wa mifugo inamaanisha kwamba ardhi inadunishwa katika maeneo makavu na yalio makavu kwa nusu katika kiwango cha haraka zaidi kuliko vile inavyofikiriwa katika kiwango cha mchakato wa asili. Tukio la ardhi kugeuka jangwa kwanza lilijitokeza kwenye nadhari ya dunia mwishoni mwa miaka ya 1960. Watu laki mbili na hamsini elfu na mamilioni ya mifugo walikufa katika kipindi cha miaka sita katika eneo la Sahel Afrika magharibi kusini mwa jangwa la Sahara.

Wataalamu wanatabiri kwamba jangwa la Sahara linatanuka kuelekea kusini kwa kati ya kilomita tano na kumi kila mwaka. Ukitilia maanani kwamba jangwa la Sahara lina upana wa zaidi ya kilomita elfu tano unatambuwa kwamba jangwa jipya linakuja kwa wingi kila miezi kumi na mbili. Shirika la Mpango wa Mazingira la Umoja wa Mataifa limekadiria kwamba dola bilioni nne na nusu zinahitajiwa kutumika kila mwaka katika kipindi cha miaka 20 ijayo kuzuia mchakato wa ardhi kugeuka jangwa.

Kuzuia kutanuka kwa jangwa barani Afrika kunahitaji usimamizi mzuri wa ardhi. Hii ina maana kupunguza shinikizo la binaadamu linalowekwa kwa ardhi kama vile uchungaji wa mifugo na upandaji wa mazao ili kwamba udongo na mimea iweze kurudi kwenye hali yake ya kawaida.

Lakini wakati idadi ya watu barani Afrika inaongezeka vinywa vinvyohitaji kula pia vinaongezeka na hiyo kuongezeka kwa mahitaji ya ardhi ilio kavu na dhaifu barani Afrika.

**Outro - Funga kipindi**

Na hapo ndio tumefikia mwisho wa mfululizo wa vipindi vyetu maalum Sikiliza na Ujifumze juu ya mazingira ambapo leo tumelenga juu ya ardhi kugeuka jangwa. Asante kwa kuwa nasi. Iwapo unataka tena kukisikiliza kipindi hiki au kuwaelezea marafiki zako nenda kwenye tovuti yetu www.dw-world.de/be .
Kwa heri.